

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KILIMO**

**Simu ya Upepo:** "KILIMO" Dodoma  
**Simu:** +255 (026) 2321407  
**Nukushi:** +255 (026) 2320037  
**Barua Pepe:** [ps@kilimo.go.tz](mailto:ps@kilimo.go.tz)  
**Tovuti:** [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)



Idara ya Utawala,  
Mji wa Serikali Mtumba,  
S.L.P. 2182,  
**DODOMA**

**TANGAZO KWA UMMA**

**UTARATIBU WA UNUNUZI NA UUZAJI WA PARACHICHI NDANI NA  
NJE YA NCHI**

Serikali imeendelea kufungua masoko mapya ya parachichi katika nchi mbalimbali ili kuchochea mkakati wa tasnia ya parachichi, kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kipato cha mkulima. Masoko ya parachichi yaliyopo ni pamoja na India, Afrika Kusini, China, Uholanzi, Uingereza, Umoja wa Falme za Kiarabu, Kenya, Ufaransa, Ujerumani na Hispania.

Ili kulinda soko la parachichi ndani, kikanda na kimataifa, Wizara ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Tasnia ya Parachichi unaopatikana katika Tovuti ya Wizara [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz). Kufuatia Tangazo kwa Umma la tarehe 04 Oktoba, 2023 na hali ya utekelezaji unaoendelea, Wizara inasisitiza wakulima, wanunuzi na wadau wote wa tasnia ya parachichi kuzingatia utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa parachichi ikiwemo kuvuna na kuuza matunda ya parachichi yaliyokomaa. Kwa kuzingatia Mwongozo uliopo na Tangazo la awali, utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa parachichi unaopaswa kuzingatiwa ni kama ifuatavyo:-

- i. Mnunuzi wa parachichi anapaswa kuwasilisha maombi ya kibali cha kununua parachichi kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo kwa anuani ya barua pepe [masoko@kilimo.go.tz](mailto:masoko@kilimo.go.tz). Maombi hayo yaainishe eneo la uzalishaji mnunuzi atakalonunua parachichi na kuambatisha nyaraka zote muhimu zikwemo usajili wa kampuni au cheti cha kuandikishwa (extract from Registrar), utambulisho wa Namba ya Mlipa Kodi (TIN certificate), *Certificate of Tax Clearance* na Leseni ya Biashara (Export license);
- ii. Baada ya kupokea maombi hayo, Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itakagua na kujiridhisha kiwango cha ukomavu wa matunda ya

parachichi katika eneo la uzalishaji lililoainishwa na mnunuzi katika maombi;

- iii. Wizara ya Kilimo itatoa vibali kwa wanunuzi wa parachichi na kuwatambulisha wanunuzi hao ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kununua parachichi katika maeneo yaliyoidhinishwa na TPHPA;
- iv. Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) itatangaza kufungua au kufunga kwa msimu wa ununuzi parachichi kwa kuzingatia viwango vya ukomavu wa tunda (dry matter content) na msimu wa uvunaji katika eneo husika;
- v. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitasimamia malipo ya wakulima kulingana na makubaliano yaliyofikiwa baina ya wakulima na wanunuzi wa parachichi walioidhinishwa; na
- vi. Wasafirishaji wa parachichi kwenda nje ya nchi wanapaswa kuzingatia viwango vya ubora vinavyohitajika katika soko husika ikiwa ni pamoja na aina ya vifungashio; na watapaswa kuomba kibali cha kusafirisha nje (export permit) kupitia mfumo wa ATMIS chini ya Idara ya Masoko na Usalama wa Chakula. Maombi hayo yatahusisha nyaraka muhimu ikiwemo kibali cha ununuzi wa parachichi kilichotolewa na matokeo ya vipimo vya *dry matter content* vilivyothibitishwa na TPHPA;
- vii. Baada ya kupata *export permit*, mnunuzi ataomba kibali cha afya ya mimea (Phytosanitary Certificates) kinachotolewa na TPHPA kupitia mfumo wa ATMIS.
- viii. Mawasiliano kwa ajili ya ufafanuzi wowote unaoweza kuhitajika yafanyike kupitia Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Wizara ya Kilimo kwa Namba ya Simu +255 733 800 200.

Imetolewa na:

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI,  
WIZARA YA KILIMO.  
06 Novemba, 2023**